**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KISANGAJI MWAKA …………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**


***Namba za Simu***
***Mkuu wa Shule 0786697092***
***Makamu Mkuu wa Shule 0715593913***
***Mtaaluma mwandamizi 0789380300***
***Matron/Patron 0752343199***



**Shule ya Sekondari kisangaji**

**S.L.P. 349**

**BABATI -MANYARA**


**Tarehe ……………………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………………………..……………………**
**S.L.P ……………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KISANGAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI MKOA WA MANYARA MWAKA………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka .................. na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari KISANGAJI ipo umbali wa Kilometa35 Kaskazini mwa Mji wa Babati utatumia Usafiri wa basi/daladala kutoka stendi kuu ya mabasi unapatikana kwa nauli ya Tsh 2000 hadi MAGUGU,Ukifika magugu utachukua usafiri wa bajaji/pikipiki kwa nauli ya Tsh 5000.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe………….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………… Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………….**.** Kuingia shuleni mwisho saa 10 jioni, ukichelewa mzazi toa taarifa kwa namba za simu ulizopewa hapo juu. Mzazi ni lazima ufike shuleni

kumkabidhi mwanao.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

*i.* Sare ya shule hii ni sketi mbili ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu kwa Wasichana rangi ya **DRAFT KUBWA NYEUSI YENYE MISTARI YA NJANO MIKUBWA NA NYEUPE MIDOGO (kitambaa kimeambatanishwa)**Mshono ni marinda sita na si vinginevyo. suruali mbili rangi ya NYEUSI kwa Wavulana **<u>zisizo bana</u>** na ziwe na turn up miguuni isiyo pungua inchi 17.

Mashati mawili meupe ya mikono mirefu;

*ii.* Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

*iii.* Sare ya Michezo ni bukta za blue na tshirt za blue Kwa wasichana na bukta za blue na T-shirt ya blue kwa wavulana

*iv.* Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

*v.* Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na khaki kwa Wavulana

Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta **ni NYEUSI zenye** mshono wa V shingoni.

*vi.* Nguo za kushindia (shamba dress) gauni moja ndefu rangi ZAMBARAU mshono wa solo na suruali DAMU YA MZEE wavulana

*vii.* Track suti rangi ya **Dark blue**

*viii.* Tai moja rangi NYEUSI ya kufunga.

*ix.* (T-shirt) dark blue zenye kola nyeupe formsix, unaweza kununua au ukikosa zitapatikana shuleni kwa gharama ya tsh 15,000/- tu.

Xii Kwa waislamu wasichana wawe na baibui moja jeusi na ushungi mweusi wa kuswalia/kuendea msikitini.

THE HEADMASTER
KISANGAJI SEC. SCHOOL
BOX 349 BABATI



**Mfano wa kitambaa cha sketi kwa wasichana**.

2.1 **Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 counter books Q4 na kalamu angalau 10 blue na 10 nyeusi.
ii. **Ream (A4)** 4 kwa mwaka au 2 kwa nusu mhula.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Scientific Calculator $F(x)991\ ES\ PLUS$
v. Godoro ft2 na1/2 kwa inchi 3.
vi. Mashuka jozi2 blue,blanket 1, foronya ya godoro1
vii. Chandarua 1cha light blue pembe nne
viii. Nguo za ndani za kutosha (zitakaguliwa)
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
x. Ndoo1 ndogo lita kumi na kubwa 1 kwa ajili ya usafi zenye mifuniko
xi. Brashi ya kusugulia sink1, reki 1, ufagio1na rubber sguizer1
xii. Sabuni ya maji lita5 na dawa ya chooni lita1
xiii. Mwanafunzi aje na BIMA ya afya ya NHIF kwajili ya matibabu.
xiv. Tranka la chuma lenye kufuli mbili kwaajili ya kuhifadhia vitu vyake

## 2.2 Michango mbalimbali

**a) Shule ya Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:Fedha ziwekwe kwenye akaunti ya shule, benki ya C R D B Jina l a akaunti KISANGAJI SECONDARY 0150599118900**

## 2.3 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya WAZIRI MKUU – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.3 Sheria na Kanuni za Shule

*i.* Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

*ii.* Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

*iii.* Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

*iv.* Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

*v.* Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya

kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Mwanao aje na vitabu kulingana na Tahasusi anayosoma mwandishi awe **Tanzania institute of Education (TIE).**

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

***2.4* Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
iv. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
v. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vi. Kufuga ndevu;

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia lainai au simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;

xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

*i.* Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
*ii.* Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
*iii.* Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
*iv.* Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

3. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Jina na Saini ya Mkuu wa Shule…………………………**

**MKUU WA SHULE**

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO U**J**UMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI .

**TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule 0712496143/0786697092
- Makamu Mkuu wa Shule 0715593913
- Mwandamizi Taaluma 0789380300
- MATRON 0752343199

**KUPIMA AFYA**

Mwanafunzi.............................................Andika ndiyo katika nafasi mbele ya
ugonjwa ambao ulikwishaugua au unaugua:

1. Kifua kikuu.........................
2. Ugonjwa wa moyo................
3. Ugojwa wa figo……………….
4. Ugonjwa wa akili……………..
5. Ajali kubwa……………………
6. 6.Pumu…………………
7. Vidonda vya tumbo……….….
8. Kifafa……………….………
9. Kupasuliwa……………………
10. Ulemavu……………………..
11. Mimba…………………………….

KWA MATUMIZI YA KIOFISI TU MGANGA MKUU WILAYA/MKOA

……………………………………………………..…………………………………
……………………………………………………

……… Tafadhali mpime mtajwa kama afya yake inamruhusu aendelee na masomo ya Sekondari kidato cha TANO. Pamoja na haya zingatia maelezo ya mwanafunzi hapo juu. MAELEZO YA MGANGA

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

JINA LA MGANGA……………………….. SAINI ………………NA

MUHURI……………………………………………
CHEO…………………………… TAREHE…………………………